**JESMA 003**

# JARIBIO LA TATU K.C.P.E
# DARASA LA NANE 2021

**KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** _____ in zao zima la mmea uzaao ndizi.

A. Kipeto
B. Chane
C. Mgomba
D. Mkungu

Jibu sahihi ni C (Mgomba)

**1** [A] [B] [C] [D] **11** [A] [B] [—] [D] **21** [A] [B] [C] [D] **31** [A] [B] [C] [D] **41** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15.** *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.*

Siku hizi ____**1**____ za afya ____**2**____ sana humu nchini. Kinyume na awali ____**3**____ watu wengi ____**4**____ baada ya kuugua, magonjwa mengi yanagunduliwa na ____**5**____ kabla ____**6**____ madhara makubwa kwa wahasiriwa. ____**7**____ wahudumu wa afya wamefunzwa ____**8**____ za kukabiliana na ____**9**____ za aina nyingi.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. viwango | B. aina | C. huduma | D. mambo |
| **2.** | A. wameimarisha | B. zimeimarishwa | C. imeimarika | D. yameimarika |
| **3.** | A. ambavyo | B. ambayo | C. ambapo | D. ambako |
| **4.** | A. walikata kamba | B. walipiga mbiu | C. walitia mrija | D. walienda joshi |
| **5.** | A. kathbitisha | B. kuthaminiwa | C. kuidhinishwa | D. kudhibitiwa |
| **6.** | A. yalete | B. yangeleta | C. yameleta | D. hayajaleta |
| **7.** | A. Aidha | B. Ama | C. Kama | D. Lau |
| **8.** | A. maarifa | B. stadi | C. hekima | D. taaluma |
| **9.** | A. maradhi | B. ukongo | C. ndwele | D. ugonjwa |

Ninakumbuka vizuri jinsi mwalimu ____**10**____ darasani ____**11**____ siku hiyo. Ulikuwa wakati wa ____**12**____ tulipomaliza tu kubugia kishuka chetu. "Sonia, njoo ofisini mwangu," akaniambia. Huku nikiwa na woga wa ____**13**____, nilimfuata mwalimu ____**14**____. Nilipoketi na kutulia, alinieleza kuwa alikuwa amempata mhisani wa kuyadhamini masomo yangu. Siku hiyo ndipo nilipojua kuwa ____**15**____.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. alioingia | B. alivyoingia | C. aliyeingia | D. alimoingia |
| **11.** | A. mwetu | B. letu | C. yetu | D. zetu |
| **12.** | A. machweo | B. mawio | C. magharibi | D. adhuhuri |
| **13.** | A. fisi | B. mkizi | C. kunguru | D. kunguni |
| **14.** | A. huyo | B. huyu | C. ule | D. wake |
| **15.** | A. daraja livuke ulifikiapo | B. Mungu akiziba hapa huzibua pale | C. mkalia kuti kavu kuanguka si ajabu | D. kila ngoma ina mchezo wake |

*Kuanzia swali la* **16** *mpaka* **30,** *jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.*

**16.** Andika wingi wa sentensi ifuatayo.
Dobi alikuletea ufagio huo.
A. Dobi walikuletea fagio hizio.
B. Madobi walikuletea fagio hizo.
C. Dobi waliwaletea fagio hizo.
D. Madobi waliwaletea fagio hizo.

**17.** Tambulisha viwakilishi vya nafsi katika sentensi.
Anakujua vizuri.
A. a, na B. a, ku
C. ku, a D. na, ku

**18.** Mkutano ulimalizika saa sita mchana. Huku ni kusema kuwa **ulimalizika,**
A. macheo. B. machweo.
C. alasiri. D. adhuhuri.

**19.** Bainisha orodha yenye **vihusishi** pekee.
A. Safi, kwao, zile, lenyewe.
B. kando, pembeni, zaidi ya, simile.
C. katika, kwenye, karibu na, dhidi ya.
D. salaale, Ala, Lo, kumbe.

**20.** Sentensi gani imetumia **kwa** kuonyesha namna ya kutenda?
A. Moshe alipongezwa kwa kupasi mtihani.
B. Tulienda moja kwa moja hadi sherehenі.
C. Mashabiki wote walishangilia kwa nguvu.
D. Mwanafunzi huyo alipelekwa kwa mwalimu wake.

**21.** Neno lipi **halifai** katika orodha hii?
A. buli B. manati
C. uteo D. chano

**22.** Kanusha: Baiskeli iliyopotea imepatikana.
A. Baiskeli iliyopotea haijapatikana.
B. Baiskeli haikupotea wala kupatikana.
C. Baiskeli ambayo haikupotea haijapatikana.
D. Baiskeli isiyopotea haikupatikana.

**23.** Mtu ambaye ana ujuzi wa kutunga mashairi huitwa,
A. manju. B. sogora
C. kungwi. D. malenga.

**24.** Andika kauli ya **kutendea** ya sentensi ifuatayo.
Juma alienda maktaba akaandika insha.
A. Juma aliandikiwa insha maktabani.
B. Insha ya Juma aliandikwa maktabani.
C. Maktabani walimwandikia Juma insha.
D. Juma aliandikia insha maktabani.

**25.** Kipi ni kitenzi kilichoundwa kutokana na nomino?
A. lima - limisha.
B. ucheshi - mcheshi.
C. wimbo - imba.
D. onea - onevu.

**26.** **Saruji** ni udongo laini inaotengenezwa kutokana na mawe, chokaa na jasi.
**Saruji** aidha ni
A. tandiko la farasi.
B. kiti katika chombo cha usafiri.
C. kanuni za lugha..
D. kazi zotw za kiufundi.

**27.** Neno lipi lina silabi saba?
A. Walitupelekea.
B. Andikia
C. Aliwasimamishia.
D. Shelabela

**28.** Akisami $\frac{3}{10}$ kwa maneno huitwa,
A. thuluthi tatu.
B. kumi kwa tatu.
C. thuluthi kumi.
D. ushuri tatu.

**29.** Andika usemi wa taarifa wa sentensi ifuatayo.
"Tutaufanya mtihani mwingine juma lijalo," mwalimu akasema.
A. Mwalimu alisema kuwa wataufanya mtihani mwingine juma lijalo.
B. Mwalimu alitaka kujua iwapo tungeufanya mtihani mwingine juma ambalo lingefuata.
C. Mwalimu alitaka kujua iwapo tungefanya mtihani mwingine Juma ambalo lingefuata.
D. Mwalimu alisema kwamba wataufanya mtihani mwingine juma lifuatalo.

**30.** **Ndoto njema haihadithiwi** ni kuwa wale wanaopenda kuifichua mipango yao kwa watu wengine. **Ndugu mbaya si rafiki mwema** ni kwa wale
A. wanaopuuza mchango wa rafiki mzuru maishani.
B. wanaopuuza uhusiano wa damu kwa sababu ya marafiki.
C. wanaothamini ndugu zao kama marafiki.
D. wanaoathiriwa na jamaa wa karibu maishani mwao.

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali kuanzia nambari* **31** *mpaka* **40**

Demokrasia ni mfumo wa utawala ambapo wanaotawaliwa huhusishwa katika takriban kila suala kabla ya uamuzi wowote kutolewa. Uamuzi wa mambo mengi upo mikononi mwa umma au wanaotawaliwa. Uongozi wa kimabavu hauna nafasi katika mfumo huu wa utawala.

Katika shule zetu hasa za upili, demokrasia inapaswa kupewa nafasi. Kila muhula, baadhi ya shule zetu za upili hukumbwa na wimbi la migomo huku wanafunzi wakilalamikia ukatili unaoendelezwa na walimu wao au viranja katika shule hizi. Iwapo demokrasia itahimizwa katika shule zetu, usawa, uwajibikaji na utulivu utashuhudiwa katika taasisi hizi za masomo. Huenda migomo tunayoshuhudia ila mara ikapungua kwa kiasi kikubwa. Nguvu za mamlaka shuleni zitaweza kudhibitiwa ili walio na nia ya kuwanyanyasa wenzao wasipate mwanya wa kufanya hivyo.

Moja kati ya njia za kuhakikisha kuwa demokrasia inadumishwa shuleni ni kuhakikisha kuwa na baraza la wawakilishi wa wanafunzi. Baraza kama hili huwajibika kwa kuwasilisha malalamishi ya wanafunzi moja kwa moja kwa mamlaka husika. Kwa mfano, ikiwa wanafunzi wana tatizo katika somo fulani, malalamishi hayo huwasilishwa kwa mwalimu husika au kwa mkuu wa idara husika bila kukawia. Suluhisho la tatizo hili hutafutwa mara moja. Wanafunzi huhisi kuwa wameridhika na hivyo huondoa hali ya wasiwasi miongoni mwa wanafunzi

Mfumo unaotumiwa na shule nyingi hivi sasa ni ule wa kutumia viranja kama viongozi wa wanafunzi. Mfumo huu hushutumiwa na wanafunzi wengi kwa sababu viranja huwa na nguvu na mamlaka kupita kiasi. Wengine wao huonekana kama miungu wadogo. Huweza kuwaamrisha wanafunzi wengine kupiga magoti, kukimbia uwanjani mara kadhaa au hata kuwacharaza viboko wapatikanapo katika makosa. Mfumo wa kidemokrasia katika utawala wa viranja ni nadra. Katika shule moja mkoani kati, wanafunzi walizua rabsha na kuwaangamiza vijana kwa kuwateketeza kutokana na nguvu hizi katika mfumo huu wa uongozi.

Wanafunzi ni viongozi wa kesho. Kutokana na mabadiliko ya kisiasa nchini na uzito uliowekewa haki za kibinadamu, itabidi wanafunzi wafunzwe kufuata mfumo unaozingatia haki na maoni ya wengi. Wasiwe na kasumba kuwa uongozi mzuri ni ule wa kiimla na wa kutumia mabavu. Ni vizuri kutii maoni ya wengine kwa sababu hata wao wana nafasi katika jamii na uhuru wa kutoa maoni waliyo nayo. Wanaohusishwa katika uongozi wa kidemokrasia huhisi kuwa wanathamani katika jamii na jambo hili huwapa motisha ya kujitolea katika majukumu ya kuboresha uongozi husika. Wao huwa na imani kuwa jamii salama zaidi na inayozingatia haki itaafikiwa siku moja katika maisha ya mwanadamu. Demokrasia shuleni huwapa wanafunzi uwezo wa kujieleza kwa ufasaha. **Vipawa hivi vikikuzwa wao huja kuwa viongozi wazuri sana katika jamii au hata katika taifa.**

**31.** Chagua maelezo yaliyo sahihi

A. Watawaliwa huhusishwa katika masuala yote kabisa katika mfumo wa kidemokrasia.

B. Katika mfumo wa kidemokrasia watawala hawawezi kuamua jambo lolote.

C. Umma huchangia kwa mengi katika mfumo wa utawala wa kidemokrasia.

D. Maoni ya wachache ndiyo yanayopewa kupaumbele katika utawala wa kidemokrasia.

**32.** Uongozi wa kimabavu ni ule ambao,

A. watawala hutumia nguvu kupita kiasi.

B. wananchi hushirikishwa katika mambo mengi.

C. serikali huleta yale wanayotaka wananchi.

D. raia ni viongozi hufanya mambo kila mtu kivyake.

**33.** Migomo katika shule zetu imekuwa ikichangiwa na,

A. viranja wanaotetea uongozi wa kidemokrasia.

B. wanafunzi wanaohisi kuwa wananyanyaswa.

C. mbinu mbaya wanazotumia walimu kufunza.

D. kuwanyima wanafunzi uhuru wa kufanya watakalo.

**34.** Ikiwa demokrasia itazingatiwa shuleni,

A. itakuwa vigumu kutekeleza sheria za shule.

B. mgogoro utazuka baina ya walimu na wanafunzi.

C. wanafunzi wote watasoma na kupita mitihani.

D. hali ya utulivu itaenea kwa urahisi.

**35.** Baraza la wawakilishi wa wanafunzi lina jukumu lipi?

A. Kuwaadhibu wanaokiuka sheria shuleni.

B. Kueleza haja za wanafunzi kwa watawala.

C. Kupinga maovu yanayoendelezwa na viongozi.

D. Kuhakikisha kuwa wanafunzi wanafunzwa ipasavyo.

**36.** Hali ya wasiwasi huzuka ikiwa,

A. suluhisho mwafaka halitafutwi kwa wakati ufaao.

B. wanafunzi wamepata matatizo katika masomo.

C. mkuu wa idara hataki kuwasikiliza viongozi wa wanafunzi.

D. wanafunzi wanajiamulia mambo bila kuwashirikisha walimu.

**37.** Msimamo wa mwandishi kuhusu uongozi ni kuwa,

A. kiongozi sharti aogopwe na kuheshimiwa na wanaotawaliwa.

B. uongozi mzuri ni ule wa kiimla na kimabavu.

C. utawala bora ni ule wa kuwahudumia wengine bali si mabavu.

D. walimu hawapaswi kuingilia masuala yanayowahusu wanafunzi.

**38.** yaliyofanyika katika shule ya mkoa wa kati iliyotajwa ni ishara kuwa,

A. viranja katika shule karibu zote wanatumia mabavu.

B. wanafunzi wamechoshwa na utawala mbaya wa walimu.

C. watu wakinyimwa haki wanafaa kuchukua sheria mikononi.

D. Uongozi usiofaa unaweza kuwa chanzo cha maafa.

39. Kulingana na aya ya mwisho,

A. wanaoshirikishwa katika maamuzi hujitahidi kuboresha utawala wao.
B. walio na tumaini la uongozi bora hufanya bidii kuvumilia dhuluma zilizopo.
C. Uhuru wa kutoa maoni huwanyima viongozi nafasi ya kuchangia utawala bora.
D. shule zote sasa zinafahamu manufaa ya mfumo wa utawala wa kidemokrasia.

40. 'Vipawa hivi vikikuzwa wao huja kuwa viongozi wazuri sana katika jamii na hata katika taifa. Ni methali gani inayofaa zaidi kuelezea kifungu hiki?

A. Mtaka cha mvunguni sharti ainame.
B. Mtoto akibebwa hutazama kisogo cha nina.
C. Ukiona vyaelea jua vimeundwa.
D. mwana mui ni dawa ya mlango.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kuanzia* **41** *mpaka* **50**

Halima alikuwa binti wa pekee katika aila ya watoto sita. Yeye ndiye aliyekuwa mziwada. Wakati wa kuzaliwa kwake, umri wa wavyele wake ulikuwa mpevu kiasi. Kule kucheza sana na kushiriki mengi na kaka zake kulimfanya kuegemea sana michezo iliyochezwa na watoto wa kiume kama vile kandanda, jungwe na miereka.

Makuzi ya Halima hayakuwa tofauti na ya maumbo zake. Alidinda kabisa kuzisuka nywele zake na badala yake alitembelea chega kwa lengo la kuzidira nywele zake tu. Binadamu nao ni ng'amba hawakosi la kuamba. Masakubimbi walieneza hili na lile kuhusu hali hii. Ilisemekana kuwa mtoto huyu alikuwa na maumbile ya kike na ya kiume. Kitoto nacho kiliendelea kujikulia tu, hakina habari kuhusu waliyodai walimwengu.

Masomoni Halima alionyesha ufarisi mkubwa katika masomo ya Hisabati na Sayansi. Wengi walistaajabia hali hii kwani haya yalionekana kama himaya ya kiume. Walimu waliutambua uhodari huu na kuendelea kumpiga msasa ili aimarike zaidi. Ama kweli, kinolewacho hupata. Alama zake ziliendelea kupaa kila uchao.

Alipojiunga na shule la upili ya wasichana ya Maendeleo wavyele wake walidhani kuwa hulka yake ingebadilishwa na kule kutangamana na mabarati pekee. Hata hivyo, hali haikuwa hivyo. Walimu shuleni walikuwa wepesi wa kutambua kipawa chake nao wakaazimia kukipalilia. Mwalimu wake wa darasa alimtafutia vitabu ainati vya masomo ya Sayansi na Hisabati. **Wembe nao ukawa ni ule ule**.

Halima alijiunga na chuo kikuu kusomea shahada ya uhandisi. Hili liliwashangaza hata kaka zake. Walianza kumwona dada yao kama mwenye dosari kubwa. Tangu lini mwanamke akaifanya kazi hii? Lo! Ukistaajabu ya Musa utayaona ya Firauni. Hata hivyo, Halima alikuwa nahodha hodari asiyeogopa mawimbi . Kwa ufadhili wa serikali, akaweza kusoma hadi shahada ya tatu.

**Mshale mzuri haukai ziakani.** Haukupita muda kaba ya Halima kuajiriwa na shirika la ndege nchini kama mhandisi mkuu. Uwajibikaji na bidii yake kazini ilimfanya kuheshimiwa na kupendwa sio na waajiri wake tu bali pia wafanyakazi wenzake. Vyombo vya habari navyo vikamsifia sana binti huyu aliyevuka vizingiti vya itikadi za kijamii na kuwa nyota iliyong'aa na kuiangazia jamii yake. Hata kaka zake **wakamhusudu** pakubwa.

**41.** Chagua maelezo **yasiyo** sahihi kulingana na kifungu
- A. Familia ya akina Halima haikuwa na mtoto wa kike.
- B. Halima alikuwa mtoto wa mwisho kuzaliwa.
- C. Wazazi wa Halima walikuwa wameanza kuzeeka.
- D. Mtoto hujifunza michezo iliyo katika mazingira yake.

**42.** Kwa nini Halima hakupenda kuzisuka nywele zake?
- A. Alizoea kuwaona wasichana walionyolewa.
- B. Hakujua kuwa wasichana hawafai kunyolewa.
- C. Hakupata fulusi zilizohitajika ili akasukwe.
- D. Aliathiriwa na yale aliyoyaona kwa kakaze.

**43.** Uvumi walioeneza masakubimbi kuhusu Halima ni kuwa,
- A. asingeweza kupata mtoto.
- B. hawezi kuolewa kamwe.
- C. alikuwa na viungo vya jinsia mbili.
- D. alikuwa mvulana.

**44.** Jukumu la mwalimu kulingana na kifungu hiki ni;
- A. kuhimiza wanafunzi kusoma masomo ya jinsia zao.
- B. kutambua na kuimarisha vipawa vya wanafunzi.
- C. kuwasaidia wanafunzi kupata alama za juu.
- D. kuwahimiza wanafunzi kupita masomo magumu.

**45.** Kulingana na aya ya tatu,
- A. wavyele waliridhishwa na mwelekeo wa Halima.
- B. Walimu walimtarajia Halima kubadili mwelekeo.
- C. Halima hakutaka kutangamanana na wasichana.
- D. Usawa wa jinsia ulizingatiwa vyema shuleni.

**46.** **'Wembe nao ukawa ni ule ule.'** Maana yake ni kuwa;
- A. aliendelea kufanya vyema katika masomo yote.
- B. aliendelea kuwashangaza wengi kama awali.
- C. aliendelea kufanya vyema katika Hisabati na Sayansi.
- D. aliendelea kupewa vitabu ili aweze kuimarika.

**47.** Halima alisomea taaluma gani chuoni?
- A. Ufundi wa mitambo
- B. Hesabu ya pesa
- C. Utaalamu wa uhazigi
- D. Uendeshaji wa ndege.

**48.** Kaka zake Halima walianza kumwona dada yao kama mwenye kasoro kubwa kwa sababu
- A. aliamua kusomea taaluma ya kiume.
- B. alichukuwa mwelekea ulioonekana kuwa kinyume na jinsia yake.
- C. alisomea mambo ambayo hata wao hawakuyamudu
- D. alikuwa amejiunga na chuo kikuu kinyume na matarajio yao.

**49.** Aya ya mwisho inaonyesha kuwa,
- A. jamii haikuridhishwa na mkondo wa Halima.
- B. wote wanaokiuka itikadi za jamii hufanikiwa maishani.
- C. ufanisi maishani kutokana na vigezo aliyo navyo mtu.
- D. vyombo vya habari vinaweza kuchangia kubadili msimamo wa jamii.

**50.** Maana ya **'wakamhusudu'** kulingan ana muktadha ni
- A. wakakerwa na hali yake.
- B. wakashangazwa naye.
- C. wakavutiwa na hali yake.
- D. wakaiga hali yake.